


# SPACE SCOOP

Bringing news from across the Universe to kids all around the world



EU UNIVERSE  
AWARENESS

## Amka na Furaha ni Muda wa Kifungua Kinywa!



Weki chache zilizopita, wanaastronomia waliangalia shimo jeusi (black hole) kwa mshangao sana, baada ya kujitokeza katika magimba na kuanza kujipatia kifungua kinywa. Sio kwa maandazi au kitafunwa kingine bali ni supa-Jupital Supa-Jupita ni gimba kubwa zaidi ya Jupita (sayari kubwa kuliko zote katika mfumo wetu ws Jua), lakini sio kubwa kutengeneza nyota. Katika kesi yetu ni kubwa mara 30 zaidi. Ili kupata uelewa mzuri Dunia inaweza kuingia ndani ya Jupita mara 1300!

Tukio: kundi la wanaastronomia kutoa European Space Agency walikuwa wamekaa usiku wakiangalia anga, wakati muale usiotarajiwa wa X-ray ghafla ulipokatiza katika vioo vya komputa zao. Walijawa na shauku ya kufahamu muale huu ulitokea wapi na kuanza kutafuta chanzo chake. Ambapo waligundua kuwa unafoka katika kiini cha galaksi unayojulikana kwa jina la NGC 4845. Galaksi hii imechunguzwa mara nyingi, lakini katika usiku huu, ilikuwa iking'a'aa mara 1000 zaidi ya kawaidal!

Mwanga wake ultoka katika sehemu uliyopashwa joto kuzunguka kiini (shimo jeusi), huku kikiachiana na kuanza kutafuna kitu cha ajabu. Shimo jeusi hili katika kiini cha NGC 4845 linakadiriwa kuwa na uzito wa karibu mara 300 000 zaidi ya ule wa Jua letu. Pia hupenda kucheza na chakula chake: kwa muda wa miezi 2-3, ilikuwa linacheza na kitu hiko cha ajabu kabla ya kukitafuna kuwa moja ya kumi ya ukubwa wake wa awali!

Unaweza kuona jinsi tukio hilo lilivyotheke, kama lilivytengenezwa kwa komputa hapa

### COOL FACT

Kuna mipaka maalum inayozunguka shimo jeusi iitwayo event horizon. Ni katika sehemu hizo ambapo kila kitu, hata mwanga ni lazima viiringie katika shimo jeusi. Hakuna kutoroka mara baada ya kuvuka event horizon!



More information about EU-UNAWE  
Space Scoop: [www.eu-unawe.org/kids/](http://www.eu-unawe.org/kids/)